



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA**

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA



Tovuti: www.hlpc.go.tz

KUFUNGULIWA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukua nafasi hii kuwajulisha Wahitimu wote wa shahada ya Maabara ya afya binadamu kuwa dirisha la maombi ya utarajali litafunguliwa **tarehe 14.11.2023** saa 4 asubuh. Aidha dirisha litafungwa **tarehe 15.11.2023** saa 9:30 alasiri. Maombi yote yatafanyika kupitia mfumo wa hprs.moh.go.tz

Mambo muhimu ya kuzingatia;

1. Wahitimu wanaoruhusiwa kufanya maombi ya utarajali ni wale tu ambao wamefaulu na kupata barua ya utambulisho kutoka chuoni.
2. Wahitimu walio soma vyuo vya nje ya nchi wanatakiwa kuhakikisha wameambatanisha barua ya utambulisho kutoka **TCU** pamoja na cheti cha matokeo au cha chuo
3. Waombaji wote wanatakiwa wawe wamefanya maombi ya usajili wa awali na usajili huo uwe umeithinishwa (**Approved**).
4. Waombaji wote wanasisitizwa kufanya maombi kwa wakati na kama anahitaji kubadilisha kituo cha utarajali atafanya ivyo kituo chenye nafasi kabda dirisha halijafungwa. Baada ya dirisha kufungwa hakutakuwepo na uwezekano wa kubadili kituo cha utarajali.

Aidha; wale wote watakaopangiwa vituo vya utarajali wanatakiwa kufika Dodoma Ofisi ya Msajili **tarehe 17.11.2023** saa 2:00 Asubuhi kwa ajili ya kupata maelekezo pamoja na nyaraka za kipindi cha utarajali. Kikao hichi wote wafike na barua za utambulisho pamoja, waliosoma vyuo vya nje ya nchi wafike na uthibitisho (Recognition award) kutoka TCU.

Ofisi ya Msajili inawatakiwa utekelezaji mwema.

Kwa maelezo zaidi piga simu 0734005777.

Imetolewa na:

Msajili

Baraza la Wataalam wa Maabara.

